JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

**Tarehe 02/06/2022**

**TANGAZO LA ZABUNI MBALIMBALI ZA UWAKALA NA NYINGINEZO**

**(1).** Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inapenda kutangazia Kampuni , taasisi, vikundi, wafanya biashara au watu binafsi wenye uwezo wa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmasahauri, kupanga kwenye vibanda / Majengo ya Halmashauri na/au kutoa bidhaa maalum/huduma kwa kipindi cha miezi 12 ambacho kitaanza tangu tarehe **01/07/2022** hadi tarehe **30/6/2023 kama ilivyoainishwa katika makundi A– H** hapa chini:-

**(A) ZABUNI ZA UWAKALA MBALIMBALI – VYANZO VIKUU VYA HALMASHAURI**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/01- LOT 1 | Zabuni ya ushuru wa Mchanga, Kokoto na Mawe |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/01- LOT 2 | Zabuni ya Ushuru wa mabasi madogo stendi ya Dunda Bagamoyo mjini |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/01- LOT 3 | Zabuni ya Ushuru wa mabasi mkubwa stendi ya Kichemchem Sanzale Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/01- LOT 4 | Zabuni ya Ushuru wa mazao ya misitu |

**(B) ZABUNI YA UWAKALA MBALIMBALI – VYANZO VINGINE VYA HALMASHAURI**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/02- LOT 1 | Zabuni ya Ushuru wa maegesho ya Ufukweni Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/02- LOT 2 | Zabuni ya ushuru wa mnada wa mifugo kata ya Fukayosi |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/02- LOT 3 | Zabuni ya Ushuru wa mazao ya Kilimo tofauti na Korosho |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/02- LOT 4 | Zabuni ya Ushuru ushuru wa maegesho ya magari, pikipiki na Bajaji kwenye Soko la Samaki la Kisasa la Bagamoyo |

**(C) ZABUNI ZA UWAKALA MBALIMBALI - USHURU WA TAKA NGUMU**

| NAMBAYA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 1 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Dunda |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 2 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Magomeni |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 3 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Nianjema |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 4 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Kisutu |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 5 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Mapinga |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 6 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Kerege |

| | |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 7 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Zinga |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 8 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Kiromo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/03- LOT 9 | Zabuni ya ushuru wa uzoaji taka ngumu Kata ya Kiromo |

**(D) ZABUNI ZA WAKALA MBALIMBALI – VYOO MBALIMBALI VYA HALMASHAURI**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/04- LOT 1 | Zabuni ya ushuru wa choo cha Soko la Samaki la kisasa Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/04- LOT 2 | Zabuni ya ushuru wa choo cha Kastamu (TRA ya zamani) |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/04- LOT 3 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Stendi ya mabasi madogo Dunda Bagamoyo mjini |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/04- LOT 4 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Stendi ya Mabasi makubwa Kichemchem Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/04- LOT 5 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Soko jipya |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/04- LOT 6 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha soko la MIVARF |

**(E) ZABUNI YA UPANGAJI KWENYE MAJENGO NA VIBANDA VYA BIASHARA**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/05- LOT 1 | Zabuni ya upangaji wa karakana ya magari na maegesho yake . |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/05- LOT 2 | Zabuni ya upangaji kwenye mgahawa wa Halmashauri uliopo kwenye stendi ya mabasi madogo Dunda Bagamoyo mjini |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/05- LOT 3 | Zabuni ya kupanga kwenye chumba Na.1 cha Biashara kilichopo kwenye Stendi ya mabasi madogo Dunda Bagamoyo mjini |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/05- LOT 4 | Zabuni ya kupanga kwenye chumba Na.2 cha Biashara kilichopo kwenye Stendi ya mabasi madogo Dunda Bagamoyo mjini |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/05- LOT 5-80 | Zabuni ya upangaji kwenye kila moja ya vibanda vinatumika **LOT 5 - 80** vilivyopo kwenye soko jipya Bagamoyo mjini |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/05- LOT 81-95 | Zabuni ya upangaji kwenye kila moja ya vibanda visivyotumika **Na 81 - 97** vilivyopo kwenye soko jipya Bagamoyo mjini |

**(F) UTOAJI HUDUMA MAALUM -ULINZI WA OFISI NA MAJENGO**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/06- LOT 1 | Zabuni ya kutoa huduma ya Ulinzi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/06- LOT 2 | Zabuni ya kutoa huduma ya Ulinzi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya na Soko la Samaki la Kisasa la Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/06- LOT 3 | Zabuni ya kutoa huduma ya Ulinzi kwenye soko la Samaki la kisasa la Bagamoyo |

**( G) UTOAJI WA HUDUMA MAALUM – USAFI WA OFISI NA MAZINGIRA**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/07- LOT 1 | Zabuni ya kutoa huduma ya usafi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/07- LOT 2 | Zabuni ya Huduma za usafi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo |

**(H) ZABUNI YA UTOAJI WA HUDUMA YA MATENGENEZO MADOGO YA MAGARI, PIKIPIKI, MITAMBO, VYOMBO VYA MAJINI, VIFAA TIBA, VIYOYOZI , POS, KOMPYUTA NA MASHINE ZA KUDURUFIA (PHOTOCOPIERS)**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/PRE/01- LOT 1 | Zabuni ya matengenezo madogo ya magari, pikipiki. Mitambo na vyombo vya majini . |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/PRE/01- LOT 2 | Zabuni ya matengenezo ya vifaa tiba kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/PRE/01- LOT 3 | Zabuni ya kutengeneza viyoyozi (Air Conditioners) |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/PRE/01- LOT 4 | Zabuni ya kutengeneza Kompyuta na mashine za kudurufia ( Photocopiers) |
| LGA/014/2022/2023/HQ/N/PRE/01- LOT 5 | Zabuni ya kutengeneza Machine za POS |

**(2) MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA ZABUNI HIZI**

1. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo.
2. Mwombaji asiwe mtumishi au diwani wa Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo
3. Mwombaji wa zabuni katika kundi **A, F au G** alipe ada ya maombi ya zabuni ya **Tshs. 100,000/=** kwa kila zabuni; fedha hizo hazitarudishwa.
4. Mwombaji wa zabuni katika kundi **B au H** alipe ada ya maombi ya zabuni ya **Tshs. 50,000/=** kwa kila zabuni; fedha hizo hazitarudishwa.
5. Mwombaji wa zabuni katika kundi **C, D au E** alipe ada ya maombi ya zabuni ya **Tshs. 20,000/=** kwa kila zabuni; fedha hizo hazitarudishwa

6. Wakala atakayeshinda zabuni katika kundi **A, B, C au D** awe tayari kukata risiti kwa wateja kwa kutumia mashine ya **POS** au mashine za POS atakazoazimwa na Halmashauri na kuwasilisha mapato kama itakavyokubaliwa kwenye mkataba

7. Wakala atakayeshinda zabuni katika kundi **A, B, C au D** atafikiriwa kulipwa **10%** ya kiasi alichokusanya kama atafikia lengo litakalokubaliwa kwenye mkataba.
8. Mwombaji ambaye ni kampuni, taasisi au kikundi aambatanishe hati maalum ya kisheria **(Special Power of Attorney)** kwa ajili ya mtia saini wake.
9. Maombi yote yaambatane na tamko la **dhamana ya Zabuni (Bid Securing declaration)**

10. Mwombaji wa uwakala wa kukusanya mapato ya Halmashauri katika kundi **A, B, C,** au **D** aambatanishe Bank statement za miezi mitatu ya **Januari, Februari na Machi 2022.**

11. Dhamana ya utekelezaji wa mkataba **"performance Security"** ya thamani ya mkataba ilipwe na wakala kwa miezi mitatu kabla ya kusaini mkataba kwa zabuni **B,C na D.**

12. Mwombaji ataje eneo anakotoka au ofisi za kampuni/Taasisi zilipo au kikundi kilipo (physical address) pamoja na kutoa namba za simu na/au barua pepe kwa ajili ya mawasiliano.

**(3) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI A au B**

1. Dhamana ya utekelezaji wa mkataba **"performance security"** ya thamani ya mkataba kwa zabuni za **kundi A** italipwa na wakala kwa miezi mitatu kabla yakusaini mkataba ambapo wakala atalipa fedha **taslimu mwezi mmoja** na dhamana ya **benki au bima** kwa miezi miwili ili kutimiza dhamana ya miezi mitatu.
2. **Mwombaji wa zabuni ya ushuru wa mazao ya misitukatika kundi A**, awe na watumishi wa kutosha na **vyombo vya usafiri** kwa ajili ya kufuatilia wanaotorosha mazao ya misitu kupitia njia mbalimbali.
3. Mwombaji wa zabuni katika **kundi B,** azingatie masharti ya yote ya jumla isipokuwa namba **3, na 5**

**( 4) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI C**

1. Mwombaji awe na leseni ya biashara au nakala ya hati ya usajili kwa taasisi au vikundi vya kijamii.
2. Mwombaji aambatanishe uthibitisho wa mlipa kodi (TIN)
3. Mwombaji wa zabuni ya mazingira awe na magari yaliyo kwenye hali nzuri kwa ajili ya uzoaji na usafirishaji taka hadi dampo au awe na uwezo wa kukodi magari ya kuendeshea shughuli hii. Mwombaji anayetarajia kukodi magari aambatishe mkataba hai wa ukodishaji magari husika.
4. Mwombaji aambatishe wasifu wa kampuni au taasisi.
5. Mwombaji wa zabuni ya usafi wa mazingira awe na mtaalamu wa fani ya afya mazingira aliyehitimu walau ngazi ya cheti aidha, vikundi vya kijamii Zaidi ya kimoja vinaweza kushirikiana kuwa na mtaalamu mmoja atakayekuwa mdhamini wao.
6. Mwombaji wa zabuni ya usafi wa mazingira aambatishe rasimu ya mpango mkakati wa usafi wa mazingira, sambamba na mpango wa kulinda afya na usalama wa wafanyakazi ikiwemo vifaa kinga na upimaji wa afya.
7. Ada ya uzoaji wa taka ngumu itatozwa kwa viwango vilivyoainisshwa katika sheria ya usafi na Mazingira ya mji mgodo wa Bagamoyo ya 2014 pamoja na mabadiliko yanayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa zabuni hii
8. Wakala atatakiwa kuhamasisha na kushiriki usafi wa mazingira wa Mwisho wa mwezi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

9. Zabuni hii itashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindanishi wa waombaji wakazi. Waombaji kutoka maeneo husika watapewa kipaumbele kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za manunuzi (PPA 2011 – kanuni ya 40, na kutangazwa kwenye gazeti la serikali (GN) namba 446 ya 2013).

**(5) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI D**

1. Wakala atakayeomba na kushinda zabuni yoyote ya **huduma ya choo katika kundi C** atakusanya kwa kutumia Mashine ya POS na kulipwa asilimia **sitini (60%)** ya makusanyo yatakayofikia lengo litakalokubaliwa katika mkataba;
2. Malipo ya **60%** yatalipwa kwa kuzingatia masharti yatakayokubaliwa kwenye mkataba

**(6) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI E: LOT 1-80**

**(1).** Mwombaji wa upangaji katika kundi hili awe tayari kulipa kodi ya pango itakayokubaliwa kwa muda wa angalau miezi mitatu

**(2).** Mwombaji aliyekuwa mpangaji wa awali jengo, chumba au kibanda cha biashara atafikiriwa zaidi kama hadaiwi kodi ya pango

**(7) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI E: LOT 81-97**

(1) Mwombaji wa upangaji katika kundi hili anatakiwa atembelee kibanda husika, alete makisio ya kukarabati kibanda husika na ataje kiasi anachotarajia kuilipa halmashauri kila mwezi wakati akiendelea kurejesha gharama zake.

(2) Mwombaji atafunga mkataba unaolingana na muda wa kurejesha gharama zake za ukarabati wa kibanda husika.

**(8) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI F**

1. Mwombaji wa zabuni katika kundi **F** awe na Leseni hai ya kutoa huduma ya usafi pamoja na **TIN/VAT** sambamba na nyaraka nyingine zitazotajwa kwenye kabrasha la zabuni.
2. Aidha mwombaji wa zabuni katika kundi **F** awe na Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni pamoja na **Memorandum and Articles of association/Extract from the Register** ili wamiliki wajulikane.
3. Mwombaji wa zabuni hii awe na mtaalam wa mambo ya usafi na mazingira.

**(9) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI G**

1. Mwombaji wa zabuni katika kundi **G** awe na Leseni hai ya kutoa huduma ya ulinzi pamoja na **TIN/VAT** sambamba na nyaraka nyingine zitazotajwa kwenye kabrasha la zabuni.
2. Aidha mwombaji wa zabuni katika kundi **G** awe na Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni pamoja na **Memorandum and Articles of association/Extract from the Register** ili wamiliki wajulikane.
3. Mwombaji wa zabuni hii awe na kibali cha kutoa huduma za ulinzi kilichotolewa na Wizara ya mambo ya ndani

**(10) MASHARTI MAALUM KWA WAOMBAJI WA ZABUNI KATIKA KUNDI H**

1. Mwombaji zabuni hii LOT 1 awe na karakana na aoneshe sifa za mafundi alio nao kwenye jedwali lilotolewa kwenye nyaraka ya zabuni hii.
2. Mwombaji wa zabuni hii LOT 2 awe na fundi sanifu au mhandisi wa vifaa tiba
3. Mwombaji wa zabuni hii LOT 3 awe na fundi sanifu umeme au viyoyozi au majokofu.
4. Mwombaji wa zabuni hii LOT 4 au LOT 5 awe na fundi sanifu wa kompyuta, machine za kudurufia au Afisa Tehama

**(11). Vitabu vya Zabuni** na maelezo mengine vinapatikana Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni , **S.L.P. 59,** Bagamoyo, kuanzia Saa **2.00** asubuhi mpaka **Saa 9.30 alasiri** (**Jumatatu – Ijumaa**)
.

**(12). Nyaraka za maombi** ziwe ni nakala **moja halisi** pamoja na nakala **ya kawaida moja, zote** zifungwe kwa **LAKIRI,** juu ya bahasha iandikwe **"NAMBA NA JINA LA ZABUNI INAYOOMBWA"**na zitumbukizwe katika sanduku la zabuni lililoko Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo baada ya kupokelewa na kusajiliwa kwenye ofisi ya katibu wa zabuni.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Katibu**
**BODI YA ZABUNI HALMASHAURI YA WILAYA**
**S.L.P 59, BAGAMOYO**

**(13). Mwisho wa kupokea maombi** ya zabuni ni tarehe **16/06/2022** saa **5.00** asubuhi. Zabuni zote zitafunguliwa muda mfupi baada ya muda huo katika ukumbi wa mikutano Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Waombaji wote wanakaribishwa katika ufunguzi kwa gharama zao.

Shauri Selenda
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**BAGAMOYO**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REV. 8/99

PO No: 00713008PO2200305

LOCAL PURCHASE ORDER

| | | | |
|---|---|---|---|
| Datie | 31 May 2022 | | |
| TO: | TANZANIA STANDARD NEWSPAPERS LTD | FROM: | BAGAMOYO DISTRICT COUNCIL |
| Payee's TIN: | 100-196-182 | Payer's Code: | 00713008 |
| Payee's Address: | P.O.BOX.9033 DAR-ES-SALAAM | Payer's Address: | S.L.P 59 |
| Region: | | Region: | Bagamoyo |

Warranti Holder

Please Supply Goods/ Services Detiailed below

| NO | ITEM DESCRIPTION | UOM | QTY | UNIT PRICE | VAT | TOTAL AMOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | kutioa tiangazo la mapatio na huduma mbali mbalii | Lumpsum | 1 | 2,124,000.00 | 0.00 | ************2,124,000.00 |

Totial Amounti Payable ************2,124,000.00

TERMS AND CONDITION:

1. Your invoices should be submitied tiogetiher witih tihe original of tihe LPO
2. The Purchase Order Number musti be quotied on all communications relevanti tio tihis order
3. 0 days witih deduction of2% and or 5% Witihholding Tax where appropriatie

Purchase Order Requesti No 00595

Requesti Prepared by [signature]

Goods/Service tio be delivered tio DED - Bagamoyo

Authiorized By DED

Expectied Datie for delivery31 May 2022

Prepared By: MSILANGA MAJEGELE KASOMA

Purchase Officer

Approved By: ARISTARCO BUGAMI NTEYE

HPMU

Ag DED 1/6/22.

1X1110

Accounting Officer

Official Seal